

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA
SHULE YA SEKONDARI KASSIM MAJALIWA**

S.L.P 125,
RUANGWA.

NDUGU

S.L.P 51,
RUANGWA.

Ndugu,

**YAH: MAAGIZO NA MASHARTI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA
SHULE YA SEKONDARI KASSIM MAJALIWA MWAKA 2021**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Ninapenda kutumia fursa hii kukupongeza sana kwa kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021 katika **Shule ya Sekondari Kassim Majaliwa**.

Shule ya Sekondari Kassim Majaliwa ni ya kutwa kwa wavulana na wasichana. Shule hii ipo katika kata ya Nachingwea na imesajiliwa kwa Namba.S4989. Shule ina walimu mahiri katika ufundishaji.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ambazo unatakiwa kuzisoma kwa makini nakuzifanyia kazi.

- (i) Fomu ya kupimwa afya ya Mwanafunzi kutoka kwenye Hospitali inayotambulika na Serikali. Mwanafunzi ambaye atashindwa kupima afya yake hatapokelewa.
- (ii) Fomu ya mahitaji muhimu ya shule
- (iii) Fomu za sheria za shule
- (iv) Fomu ya taarifa za Mwanafunzi na Mzazi
- (v) Fomu ya kiapo cha uraia kama hauna cheti cha kuzaliwa ipitishwe mahakamani.

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 na masomo yataanza siku hiyo. Nafasi yako itatunzwa kwa muda wa wiki mbili(02) tu tangu tarehe ya kufungua shule na baada ya haspo nafasi hiyo itajazwa na mtu mwingine na wewe utachukuliwa hatua za kisheria iukiwemo kufikishwa mahakamani.

Nakutakia maandalizi mema namaisha mapya ya Sekondari.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KASSIM MAJALIWA KWA
ELIMUBORANA MALEZI MEMA!**

.....
**IRINE FULKO KOMBA
MKUU WA SHULE**

NAMBA YA SIMU: 0786-361592

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

1. Sare za Shule (Wavulana)

- a) Wanatakiwa kuwa na Suruali mbili (2) za kijani zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo. Suruali inatakiwa iwe na mkunjo kwa chini na wala isiwe modo.
- b) Mashati meupe mawili(2) yenye mikono mifupi na yenye kola shingoni.
- c) Awe na sweta moja (01) rangi ya kijani lililofumwa.
- d) Viatu vyeusi vya ngozi (vya kufunga na kamba) jozi mbili(02). Viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vyenye visigino virefu.
- e) Soksi nyeupe jozi mbili (02).
- f) Nguo na viatu vya michezo.(Flana nyeusi na bukta nyeusi).

2. Sare za shule (Wasichana)

- (a)Wanatakiwa kuwa nasketi mbili za kijani zenye mshono wa **rinda boksi**. Sketi iwe ndefu kupita magoti na ishonwe kwa unadhifu na sio kwa mapambo.
- (b)Mashati meupe mawili(02) yenye mikono mifupi na yenye kola shingoni.
- (c)Awe na sweta moja(1)rangi ya kijani lililofumwa.
- (d)Viatu vyeusi vya ngozi (vya kufunga na kamba) jozi mbili (02). Viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vyenye visigino virefu.
- (e)Soksi nyeupe jozi mbili(02).
- (f)Nguo za michezo ni tracksuit nyeusi
- (g)Kwa wale wanaohitaji kuvaa HIJABU utaratibu ni kama ifuatavyo:

i.Sketi

- Sketi inatakiwa iwe na urefu unaofika katika vifundo vya miguu.
- Iwe pana.
- Isiwe nyepesi

ii.Blauzi(Nusu kanzu)

- Iwe na mikono mirefu isiyofunika viganja vya mikono.
- Iwe pana (isibane)
- Iwe ndefu inayoshuka chini ya makalio(isiwe kama gauni)
- Isiwe nyepesi

iii.Kitambaa cha kichwani (**ushungi**)

- Kiwe kipana.
- Kiwe kirefu kisichofunika viganja vya mikono.(kiishie kwenye vifundo nya mikono)
- Kisifunike uso
- Kisiwe chepesi

NB:Kitambaa cha kichwani(ushungi) na bilauzi (nusu kanzu) zinatakiwa zishonwe kwa kitambaa cheupe kinachojulikana kwa jina la HALUA.

3.Fulana za shule zinapatikana shuleni kwa kununua.

4.Vifaa vya usafi

(a) Fagio mbili za chelewa

(b) Jembe moja lenye mpini

(c)Panga moja

(d)Reki moja

(e)Ndoo ndogo moja

(f) Fyekeo moja

(g)Fagio laini la dukani

5.Mahitaji kwa ajili ya taaluma.

(a)Daftari 10 za Quire mbili(2) au tatu(3)

(b)Kalamu za wino wa bluu au mweusi na kalamu ya risasi(penseli)

(c)Mkebe mmoja wa vifaa vya hisabati (Mathematical set)

(d) Kamusi ya kiingereza (English to English Dictionary) na Kamusi ya Kiswahili kwa Kiswahili

(e) Ream moja A4 kutokana na makubaliano ya wazazi kikao kilichofanyika tarehe 30/07/2020.

6.Mahitaji ya chakula

Kwa kuwa ni lengo letu kuhakikisha mwanafunzi anapata chakula cha mchana hapa shuleni, utaratibu wa kuchangia uko kama ifuatavyo:

i.Mahindi kg 80 kwa mwaka. Unaruhusiwa kulipa kilo 20 kila baada ya miezi (3) kwa awamu nne (4) kwa mwaka.

ii.Mboga Kg 32 kwa mwaka. Unaruhusiwa kulipa kg 8 kwa awamu nne(4) yaani kila baada ya miezi(3).Mboga inayotakiwa ni MAHARAGE pekee.

iii.Mafuta ya kupikia lita moja(01) kwa mwaka ambayo hulipwa mara moja

iv.Chumvi nusu kilo kwa mwaka.

v.Fedha za kulipa mpishi,kusaga na kununua vifaa vya kupikia Tshs.15,000/=Hii hulipwa mara mbili kwa mwaka.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
RUANGWA DISTRICT COUNCIL

KASSIM MAJALIWA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 125,
RUANGWA.

DATE.....

REF. No.....

THE MEDICAL OFFICER.

.....
.....
.....

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF

MR.....

Please Examine the above named pupil and give us a regarding his/her suitability for Secondary School studies.

1. Pupil's full name
2. Blood.....
3. Stool.....
4. T.B test.....
5. Syphilis test.....
6. Urine examination
7. Eye test.....
8. Chest.....
9. Ear.....
10. Spleen.....
11. Abdomen test.....
12. Pregnant test (girls only).....

I certify that the above pupil is suitable/for studies

If unsuitable please give reasons.....
.....
.....

Name of MEDICAL Officer.....

Signature of Medical Officer.....

Date.....

Official Stamp.....

HATI YA KIAPO CHA KUZALIWA

HATI YA KIAPO KUHUSU NDUGU.....

Mimi.....

Nathibitisha kwa kiapo na kutamka ifuatavyo:

Kwamba mimi ni.....(taja kazi)

1.Kwamba mimi ni baba/mama/ndugu wa karibu wa.....ambaye alizaliwa tarehe.....mwezi.....mwaka.....katika kijiji cha.....kilichopo wilaya ya.....nchini.....Tanzania.

2.Kwamba mimi nilikuwa naishi katika kijiji hicho wakati wa kuzaliwa kwa.....nalikumbuka tukio hilo.

3.Kwamba kuandikishwa kwahakukufanyika muda wa miezi mitatu na ukweli kwamba kuandikisha huko hakukuwana lazima.

.....

Sahihi ya anayetoa Tamko.

Ameapishwa mbele yangu hapa.....leo tarehe.....

.....

Sahihi ya anayetoa Tamko.

Ada Tshs.....E.R.V NO.....ya tarehe.....

Futa isiyohusika

SHULE YA SEKONDARI KASSIM MAJALIWA
FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI NA
HABARI ZA MZAZI NA MWANAFUNZI.

SEHEMU A: HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili (kama kwenye mtihani).....
2. Tarehe ya kuzaliwa
3. Kabila
4. Mahali na Wilaya alipozaliwa
5. Shule alipomaliza Darasa la Saba /Kidato cha Nne
6. Kidato anachokuja kuingia
7. Michezo anayopendele

NO	JINA LA MCHEZO
I	
II	
III	
IV	
V	
VI	

Kazi yoyote ya uongozi aliyowahi kufanya kama vile. Kiranja,Kiongozi wa Kwaya,Ngoma Michezo n.k

	UONGOZI	SHULE	MWAKA
i			
ii			
iii			
iii			

Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kamili na za ukweli

Tarehe saini.....

HABARI ZA MZAZI

SEHEMU B:

Jina kamili.....

Kazi.....

Nyumbani.....

Kata.....

Tarafa.....

(a) Anwani ya Mzazi/Mlezi

(b) Namba ya simu/.....

Dini

Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo.....

Ninaahidi kushirikiana na Walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya kusoma.

MimiMzazi/Mlezi ninathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi

Tarehe saina.....

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha unatakiwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- c) Kutimiza kwa makini maandalio ya Jioni (Preparation)-Kwa mwanafunzi wa bweni
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i) Wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele
- j) Shule haimfungi Mwanafunzi kuamini katika imani yake ila kwa muda maalum na siku maalum
- k) Kuhudhuria roll-coall saa 12:00 jioni kila siku na muda mwingine wowote ambao Mwl. WaZamu/Bweni ataona kuna umuhimu wa kufanya hivyo.(Kwa wale wanafunzi wa bweni)
- l) Hairuhusiwi kutoka nje ya shule bila ruhusa
- m) Hatakiwi kuja na nguo za nyumbani
- n) Ajapo kuripoti, aje na Mzazi. Bila kuja na Mzazi hatapokelewa
- o) Ni marufuku kuendesha ibada wakati wa masomo

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule.

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevyo kama vile uvutaji bangi ,cocaine, mirungi, kubeli n.k.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuo au Kuolewa
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
10. Kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Mwanafunzi kuwa na **simu ya mkononi**
14. Mwanafunzi atakaye kutwa anachafua kuta za shule atalazimika kulipa ndoo (1) ya rangipamoja na Tshs 20,000/= za ufundi ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

UNATAKIWA KUSAINI HAPO CHINI KUTHIBITISHA KWAMBA UMEZISOMA SHERIA NA KWAMBA UKO TAYARI KUZIFUATA IPASAVYO

JINA LA MWANAFUNZI.....

SAHIHI YA MWANAFUNZI.....

TAREHE.....

MKATABA WA MWANAFUNZI KUHUSU KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Miminimeyasoma kwa makini maelezo haya ya kujiunga na shule. Kwa hiari yangu nakubaliana nayo. Naahidi nitaheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule na miongozo mbalimbali itakayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha naahidi kuwa kwavyovyote vile sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai nikiwa shuleni au nje ya shule.

Endapo nitavunja sheria, kanuni, taratibu za shule, kushiriki katika migomo, fujo na kutenda makosa ya jinai, basi nichukuliwe hatua ya stahiki kulingana na kosa nitakalokuwa nimefanya.

Saini ya Mwanafunzi

Saini ya Mzazi.....

Saini ya Mkuu wa shule